**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 25 Agosti 2007**

**Waliohudhuria**
Abdallah Fiki Ally
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishekh
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frederick John Frederick
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kassim Bakari
Lameck Charles
Patrick Masinga
Paulo Atibu Hatibu
Rahma Ali
Ramadhani Rajabu Nyengo
Rashidi Saidi Karanji

**Mradi wa Usalama wa Baiskeli / Mfuko wa Kumbukumbu wa Wamba**
Ally said Mohammed aliarifu kwamba Jumatatu yeye na Bwana Mwenguo walifuatilia na kupata barua ya utambulisho kutoka UWABA kwa ajili ya maombi ya mfuko wa kumbukumbu wa Wamba. Paulo alikwenda HUWATA kuchukua barua na cheti cha usajili toka HUWATA. Elaine alituma kwa email mchanganuo na viambatanishi kwenye anuani aliyopewa Jumanne. Hakupata jibu lolote na hivyo alijaribu kumpigia simu kwa namba ya Marekani aliyopewa ili kuthibitisha kama ilipokelewa, lakini alipata jibu la mashine la Profesa Osili. Atafuatilia tena wiki hii kuhakiki kama ilipokelewa.

**Guta**
Siku ya jumatatu Juma na Elaine walichukua benki na kumpa Jumanne afanye ukarabati wote wa guta na kununua vipuri. Jumanne alifanya kazi hiyo na guta sasa liko tayari kwa kazi. Litakusanya pesa katika wiki na Jumanne ataanza kuiteta Tsh 7000/= kila wiki jumamosi ijayo.

**Msafara wa Baiskeli**
Jumatatu Eline na Juma walikwenda kumwona mbunge wa Ilala Mh. Azzan Zungu. Tulimpongeza kwa kutumia baiskeli Bungeni na tulimtaarifu juu ya msafara wa baiskeli na kumwomba awe mgeni Rasmi. Pia alisema amekubali kuwa mgeni rasmi na alitunga mkono kuhusu msafara. Aliahidi kutusaidia kupata ufadhili na pia angesaidia kupata eneo la Mnazi mmoja bure. Alisema. Tufuatilie kwake ndani ya wiki moja. Elaine na Juma walikutana na Selemani Majembele wa AALOCOM wakati wanatoka kikaoni ambaye alikuwa amechelewa, wakati huo huo Jax wa CHABADA hakuja.

Elaine na Juma walikwenda katika kampuni ya Bakhresa kariakoo na waliambiwa Bw. Bakhresa alikuwa TAZARA. Kulitokea mzozo mkubwa kati yetu na walinzi wa Bkhresa TAZARA ambao walitaka kuturuhusu kuonana na mtu yoyote. Tulimpigia simu Bw. Lawrence (ambaye hakuwepo pale) ambaye katibu wa Bw. Bakhresa na hakuwa na msaada wowote katika kuturuhusu hadi tulipompigia simu mara tatu. Tulipoingia tuliongea na Bw. Abdul ambaye alitoa ushirikiano na alikuwa msaada na kasha alikwenda kwa Bw. Bakhresa na ombi letu la ufadhili wa maji ya kunywa na matangazo.alirudi na kusema Bw. Bakhresa atachangia chupa ya lita moja 600 za maji ya kunywa lakini sio matangazo. Tulimshukuru sana na kuahidi kumwandikia barua ya shukrani. Tulipewa namba ya simu ya Bw. Abdul ili kufuatilia namna ya kuchukua maji ya kunywa msafara ukikaribia.

Elaine alifuatilia kwa simu wafadhili wengine muhimu Ultimate Security walikiri kupokea barua yetu lakini meneja hakuwa tayari kufadhili msafara. Knight Support walimwambia aendelee kuwapigia simu siku ya nyingine. Celtel walisema bado wanafuatilia barua yetu na watajibu mapema. Mmoja wa msafara wa ubalozi wa uchina alisema ameiona barua yetu na imepelekwa kwa Balozi, lakini katibu wa Balozi alisema hajaiona barua hiyo hivyo Elaine aliituma kwa email tena.

Elaine alisema familia yake imekubali kuchangia Tsh 250,000/= kwa ajili ya msafara. Alimpa Juma pesa hiyo ili aiweke benki.

Kwa kuwa vipaumbele vya awali ni matangazo na zawadi za bahati nasibu, ilikubalika kwamba kundi la wanachama liende ubalozi wa Uchina siku ya Jumatatu asubuhi (kuondoka magomeni ni saa 2 asubuhi) ikifuatiwa na kumuona Bw. Mengi (IPP Media) kwa mara ya kwanza.

**Ofisi**

Ally saidi Mohamed aliweka rafu itumike kama sehemu ya kutunzia majarida. Kwa vile karatasi zingeweza kuanguka kirahisi, alisema ataweka vibao ili kuzuia. Pia alisema amebaki na pesa ya kutosha kutengeneza meza na droo zake. Pia atatengeneza fremu kwa ajili ya cheti cha usajili.

Eline alileta picha na dondoo kutoka katika tovuti ya UWABA ili ziwekwe kwenye ubao wa matangazo na Ally Mohammed aliziweka. Wanachama walisisitizwa kuleta michoro na matangazo (makala) kwa ajili ya kuwekwa kwenye ubao.

Paulo alisema tutoe picha ya wanachama wote katika gazeti la Dar leo.
Elaine alisema ametuma email kwa IBike, Joey na Mathew kuwataarifu kuhusu maendeleo ya ofisi.

**Sanduku la Barua**

Juma aliangalia sanduku la barua la kaka yake Mejah siku ya Jumatatu, lakini hakukuwa na barua, ikimaanisha kuwa hakukuwa na majibu ya barua zetu.

Jumanne aliuliza kama wataweza kupokea barua zao binafsi kupitia UWABA kwa wasio na masanduku ya barua na ilikubalika.

**TANROADS**
Elaine alisema atafuatilia kwa wakala wa Barabara wiki hii ili kurekebisha ratiba ya mkutano wetu na wao.

**Vitambulisho**
Sosthenes alichora nembo ya guta na baiskeli ya tairi tatu ya walemavu na kumpa Elaine siku ya Jumatatu ambaye aliiskani na kuiweka kwenye vitambulisho. Pia aliweka anuani ya posta na mahali UWABA ilipo kwenye vitambulisho, lakini hakuleta nakala kwenye kikao.

Frederick alisema kuwa vitambulisho lazima vitiwe saini na wanachama. Ilikubalika hili lifanyike japo hili lilimaanisha kwamba vitambulisho vilitakiwa kuwa vimeshachapishwa, vitaletwa kwa wanachama kasha kuwekewa magamba badae.

Ilikubalika kwamba watu lazima walipie vitambulisho kabla ya picha zao kuchukuliwa ilikuepuka vimbulisho kuchapwa kwa wanachama ambao hawawezi kuvilipia au kuvichukua.

**Tawi la Temeke**
Ilijadiliwa juu ya kuanzisha tawi Temeke kwa kuwa kuna wapanda baiskeli wengi Temeke ambao hawawezi kuja Mabibo mara kwa mara kwenye vikao. Ilikubalika kwamba Paulo na Fredrick wanoishi Temeke wafanye utafiti kuhusu sehemu nzuri ya kufanyia vikao kwa tawi Temeke. Elaine atachapisha vipeperushi kutangaza kikao cha kwanza cha tawi la Temeke ndani ya wiki chache na kuwapa Paulo na Fredrick ili wavisambaze.

**Mengineyo**
Ilijadiliwa kwamba UWABA iwe na mhuri. Paulo alisema atachunguza bei ya mhuri utakaokuwa na nembo na anuani.

Ilijadiliwa kwamba UWABA iwe na fulana ya bendera ili ziwekwe kwenye baiskeli na ziuzwe kwa wanachama. Fredrick alisema atachunguza gharama za fulana zilizochpwa.